

Uhawilishaji wa Fonimu za Kihehe na Athari zake katika Ujifunzaji wa Kiswahili Sanifu kama Lugha ya Pili

Mwaija Ngenzi

Mhadhiri Msaidizi, Chuo Kikuu Kishiriki Katoliki Mbeya

mwaijangenzi2@gmail.com

Ikisiri

Makala hii imechunguza uhawilishaji wa fonimu za Kihehe na athari zake katika ujifunzaji wa Kiswahili Sanifu kama lugha ya pili (L2). Data za makala hii zilikusanywa kutoka kwa wajifunzaji lugha jamii ya Wahehe ambao Kihehe ni lugha mama yao. Data za msingi za makala hii zilikusanywa kwa mbinu za masimulizi ya hadithi, uchambuzi wa nyaraka na jaribio lenye maswali ya orodha chunguzi. Uchambuzi sanifu wa data uliongozwa na nadharia ya Usasanyuzi Linganishi. Matokeo ya data za makala hii yanaonesha kuwa uhawilishwaji wa fonimu za Kihehe katika Kiswahili Sanifu, husababisha athari katika lugha hiyo. Athari zilizobainika ni urefushwaji wa matamshi ya maneno ya Kiswahili Sanifu; kuathiriwa kwa maana za maneno; na mabadiliko katika baadhi ya fonimu za Kiswahili Sanifu. Ili kuondoa au kupunguza athari hizo, makala hii imependekeza wajifunzaji lugha kupewa mazoezi ya kutosha ya somo la Kiswahili ambayo yatasaidia kupata maarifa zaidi ya lugha ya Kiswahili Sanifu.

Dhana za Msingi: Lugha ya kwanza, lugha ya pili, Kihehe, fonimu

Utangulizi

Uhawilishaji ni uhamishaji wa ujumbe au mawazo kutoka lugha moja kwenda nyingine kwa njia ya maandishi au mazungumzo (BAKITA, 2017). Katika muktadha wa makala hii, neno uhawilishaji limetumiwa kumaanisha mchakato wa uhamishaji wa fonimu kutoka lugha moja kwenda nyingine. Kihehe na Kiswahili ni lugha za Kibantu zinazozungumzwa nchini

Tanzania. Kihehe kinazungumzwa Kanda ya Nyanda za Juu Kusini katika Wilaya za Iringa Vijijini, Iringa Mjini, Mufindi, na Kilolo mkoani Iringa (Madumulla, 1995). Kihistoria, Kiswahili kina mtagusano na lugha nyingine za Kibantu na zisizo za Kibantu. Baadhi ya lugha zisizo za Kibantu zilizotagusana na lugha ya Kiswahili ni Kiarabu, Kiajemi, na Kireno (Mitellell na Myles, 2004). Kadhalika, lugha ya Kiswahili imeingiliana sana na lugha nyingine za Kibantu kama vile Kihaya, Kijita, Kisiha, Kizigua, Kiigembe, Kimakunduchi, na Kihehe (Rubanza, 1979; Mochiwa, 1979; Massamba, 1986; Mukuthuria, 2004, Khamisi, 2012; Kanake, 2013; na Kileo, 2017).

Kwa kawaida, mtagusano wa lugha husababisha uhawilishwaji wa elementi za lugha moja kwenda lugha nyingine (Massamba, 1986; Mukuthulia, 2004). Lugha za Kiswahili na Kihehe zimekuwa katika mtagusano kwa kipindi kirefu. Kutagusana kwake kunaweza kusababisha uhamishaji wa baadhi ya fonimu za Kihehe kwenda katika Kiswahili Sanifu. Kwa mujibu wa TUKI (1990), fonimu ni kipashio kidogo kabisa cha kifonolojia kinachobadili maana ya neno. Fonimu ina sifa ya kuweza kuyatofautisha maneno kimaana. Hii ina maana kuwa ukibadili, kuongeza au kudondosha fonimu katika neno, maana ya awali ya neno husika inaweza kupotea au kubadilika (Obuchi na Muhwana, 2015). Kwa hivyo, kutokana na mwengiliano huo wa fonimu za Kihehe katika Kiswahili, mwandishi wa makala hii ameona ni vyema kufanya uchunguzi ili kujua namna uhawilishwaji wa fonimu za Kihehe unavyoathiri lugha ya Kiswahili Sanifu.

Nadharia ya Utafiti

Nadharia ya Usasanyuzi Linganishi (NUL) iliyoasisiwa na Lado (1957) ilitumika kuongoza uchambuzi wa data za makala hii. Nadharia hii inahusu ujifunzaji lugha ya pili ambayo hulinganisha na kulinganua lugha mbili tofauti kwa madhumuni ya kuonesha kufanana na kutofautiana kwa lugha hizo. Kwa mujibu wa nadharia hii, matokeo ya ulinganisho huo hutumiwa na walimu wa lugha kuimariswa ufundishaji wa L2. Mwanzoni, nadharia hii ilitumika kulinganisha lugha mbili au zaidi katika hatua zake za kimaendeleo, lakini baadaye ilitumika kulinganisha lugha hizo katika vipengele vya kifonolojia ili kubainisha utofauti na ufanano wa lugha hizo. Kwa mujibu wa Lado (ameshatajwa), NUL hutoa mwongozo wa kuhuchunguza jinsi L1 inavyomwathiri mwanafunzi ajifunzaye L2 katika vipengele vya kiisumu kama vile fonolojia, mofolojia, sintakisia, na semantiki. Athari za L1 kwa wajifunzaji wa L2 zinaweza ama kurahisisha jitihada za ujifunzaji au kukwamisha. Katika makala hii, NUL imesaidia kulinganisha fonimu za lugha ya Kiswahili Sanifu na Kihehe. Ulinganishaji huo umesaidia kubainisha fonimu za Kihehe zinazohawilishwa katika mchakato wa ujifunzaji lugha ya Kiswahili Sanifu na athari zake.

Methodolojia

Utafiti huu umechunguza uhawilishaji wa fonimu za Kihehe unavyoathiri lugha ya Kiswahili Sanifu katika mchakato wa ujifunzaji lugha kwa kutumia uchunguzi kifani na mkabala wa kitaamuli. Sampuli ya utafiti huu ilihuisha wanafunzi ishirini na wanne (24) na walimu wanane (8) kutoka katika shule nne za msingi zilizoteuliwa kwa njia ya usampulishaji lengwa wa kipekee na usampulishaji nasibu wa kubahatisha. Data zilikusanywa kwa njia ya masimulizi ya hadithi, uchambuzi wa nyaraka, na jaribio lenye maswali ya orodha chunguzi.

Matokeo ya Utafiti

Uwasilishaji wa data za makala hii umegawika katika makundi mawili. Kundi la kwanza linahusu fonimu za Kihehe zinazohawilishwa katika ujifunzaji wa Kiswahili Sanifu, na la pili linahusu athari za uhawilishwaji wa fonimu za Kihehe katika ujifunzaji wa Kiswahili Sanifu kama L2.

Fonimu za Kihehe zinazohawilishwa katika ujifunzaji wa Kiswahili Sanifu

Matokeo ya utafiti yanaonesha kuwa lugha ya Kihehe, kama zilivyo lugha nyingine za Kibantu, ina fonimu za aina mbili ambazo ni irabu na konsonanti. Kwa mujibu wa data za makala hii, Kihehe kina fonimu za irabu tano (5) ambazo ni /a/ /e/ /i/ /o/ na /u/ na konsonanti ishirini (20) ambazo ni /p/ /b/ /t/ /d/ /k/ /g/ /ʃ/ /f/ /v/ /s/ /z/ /h/ /m/ /n/ /ŋ/ /l/ /w/ /y/.

Irabu za Kihehe zinazohawilishwa katika ujifunzaji wa Kiswahili Sanifu kama L2

Matokeo ya utafiti yanabainisha kuwa irabu za Kihehe zinazohawilishwa katika ujifunzaji wa Kiswahili Sanifu ni irabu fupi zilizowekwa toni na kurefushwa kimatamshi. Hili limebainika kupitia data ifuatayo ya masimulizi ya hadithi iliyochukuliwa kutoka kwa mmoja wa watafitiwa wanafunzi.

Hadithi Na. 1

“Apo samáni sá kále palikuwépo na mufwálume mumója aliyeítwa mufwálume awáfu. Mufwálume wúyu aliísi katika kijíji cha mikochéni katika múji wa Yelusalému. Mufwálume wúyu aliwonekána kuwatésa sána laia wáke wakulíma pamója na wafugáji. Siku mója mufwálume wúyu alitafúta nzíya ya kuwawúwa fijána wóte wa kijíji kiíle, kwani aliofia kwamba watawésa kumuyang’ánya madaláka yáke. Ambápo aliwaíta fijána wóte akawambíya fijána wángu ninapáswa kuwápa mutiyáni ambápo atakayefawúlu atamuwówa bindi yángu Uba, na nitamujéngea nyúmba kúbwa. Lakíni kwa wale watakaoféli mutiyáni uwo watauwáwa mbéle ya laíá wángu wóte. Fijána wóte

walilusíwa kwénda kutafúta mutiyáni uwo kwa síku tisíni. Kijána mumója alijitokésa akamwambíya mufwálume, wéwe mufwálume wángu mutukúfu, naaídi kufwawúlu mutiyáni **wáko** na nitamuówówa bindi yáko Uba....!”

Chanzo: Uwandani (2020).

Data zinazotokana na masimulizi ya hadithi Na. 1 zinaonesha fonimu mbalimbali za irabu za Kihehe ambazo wajifunzaji wa lugha huzihawilisha katika Kiswahili Sanifu. Katika masimulizi hayo ya hadithi, maneno yenye irabu za Kihehe zenye toni zinazohawilishwa katika ujifunzaji wa Kiswahili Sanifu yamebainishwa kwa hati ya wino mkolezo. Kama inavyoonekana katika Kielelezo Na. 1, irabu za Kihehe zilizobainika kuhawilishwa katika ujifunzaji wa Kiswahili Sanifu ni irabu fupi zenye toni zilizorefushwa kimatamshi (ufafanuzi kuhusu urefushwaji wa irabu umetolewa katika kipengele cha “urefushwaji wa matamshi ya irabu”. Hili linathibitika kupitia data ya hadithi Na. 1. Irabu hizo ni /á/ /é/ /í/ /ó/ na /ú/. Baadhi ya irabu zilizorefushwa kimatamshi zimeoneshwa katika Mifano Na. 1 – 5. Katika data hiyo, silabi zenye na toni, zimeoneshwa kwa kurefushwa matamshi kama ambavyo wajifunzaji huzitamka.

Jedwali Na.1: Irabu Zinazohawilishwa katika Kiswahili Sanifu

	Tahajia ya Neno	Matamshi ya Kihehe	Matamshi ya Kiswahili Sanifu
1 (a)	zamani	/sama:ni/	/za'mani/
(b)	zaa	/saa/	/za/
2 (a)	palikuwepo	/palikuwɛ:po/	/paliku'wɛpo/
(b)	kwenda	/kwɛ:nda/	/kwɛnda/
3 (a)	njia	/nzi:ja/	/njija/
(b)	kijiji	/kijii:ji/	/ki'ji:ji/
4 (a)	wote	/wɔ:te/	/'wɔ:te/
(b)	pamoja	/pamɔ:ja/	/pa'mɔ:ja/
5 (a)	mtu	/mu:tu/	/'mtu/
(b)	mtukufu	/mutuku:fu/	/mtu'kufu/

Chanzo: Data za Uwandani (2020)

Data Na. 1 - 5 zinaonesha irabu za Kihehe zenyé toni zinazohawilishwa katika ujifunzaji wa Kiswahili Sanifu. Katika data hizo, kuna uhawilishwaji wa irabu /á/ /é/ /í/ /ó/ na /ú/ unaobainika kuitia maneno mbalimbali kama yanavyoonekana katika data zilizooneshwa katika hadithi Na. 1. Aidha, katika data hizo, mtafiti ameonesha namna maneno hayo yenye toni yanavyotamkwa na wajifunzaji lugha.

Konsonanti za Kihehe zinazohawilishwa katika ujifunzaji wa Kiswahili Sanifu kama L2

Kwa mujibu wa data zilizopatikana kwa njia ya usimulizi wa hadithi, uchambuzi matini na jaribio, konsonanti za Kihehe zilizobainika kuhawilishwa katika Kiswahili Sanifu ni tatu ambazo ni /s/, /f/, /l/. Katika Kielelezo Na. 1 tunaweza kuona konsonanti hizo kuitia data zilizopatikana kwa njia ya uchambuzi matini ya mazoezi ya wanafunzi darasani.

Kielelezo Na. 1: Uchambuzi Matini

RISALA

25-06-2020

Kuandikika rsala igiyordi
maneno 200 ndani ya clftari
Langu.

Risaala

Ndugu mugeeni @asimi. A
awali ya ydote tunapeenda
Kutooa sukuu@ani Geetu kwa
ako na wageeni Woote uli
Wo andamaana naiwo. Tuna
Sukuu saana kwa kufuka
aapa katiika suule yeetu
Ndugu mugeeni @asimi
Kipekee saana tunaku
Sukuu kwa kutujengeey
a sibitaali ya suule am
baayo ata wana kijiji
Wana nu fwai@ka naay o.
Tuna seema Saande sac
na na tunausamini sac
na mchaango wako kweeto.

Ndugu mugeeni Paasimi
Suule ii iliyasiza muna
mo Mwaaka wa 1974 ikiwa
na jumula ya wanaquuzi
120 na waalimu wanaane
Kati ya wanaquuzi 90 wa
nawaake wali kuuws 40
na wanawuume 80. Suule
ilikuwa na ~~f~~yumba ~~f~~
taatu tu ~~f~~yaa macka
sa

Ndugu mugeeni Paasim
i, adileo ii suule ii ina
wanaquuzi jumula ya 412
dalasa la kwaaza adi
la saaba. Wanawaake
wa po 200 wanawuume
212. Suule ina jumula
ya waalimu 21.

~~Ndugu mugeeni Paasi
mi, kila mwaaka suule~~

hufa wulisa watoto wasi
taani 38-40 kwendwa selko
ndaa^①

Aya kweeta ni mafua
nikiiyo makubwa mano.
~~file file~~ idaadi ya ~~f~~yuu
mba jya madalaasa i me
o nge~~see~~ka kutooka mada
laasa mataatu aadi ma
dalaasa 18.

Ndugu mgeeni Oasimi
pamoja na mafua nikiiyo
aya suule yeetu ina cha
nya mootho nyiringi kwaaza
uchakaa^② na uboofu wa
miundo mbiini pili uchaa
che wa madalaasa amba
ayo aya kii~~ti~~ idaadi ga
wanafunzi tulwonau
waatimu uuja na kuwond
ooka na kubaa~~ti~~ wachaa



che tu, tatu ndugu mugeeni laasimi, suule yeetu ina sida ya madawaati, fliti fya walimu na Nyumba fya kuuisi waalimu.

Ndugu mugeeni (kasi) mi mwisho kwa heshima na taatima tunawoomba utuwekee lijiwe la musi ingi kweenye jeengo jupy a la nyumba ya muallimu mukuu. Sande kwa kutsi kilici za. ✓

Kasi nazi! Rekebishi martamshi yako. Kiswahili shaka kibovu.

Chanzo: Data za Uwandani (2020)

Kielelezo Na. 1 cha uchambuzi matini, kinaonesha konsonanti za Kihehe zinazohawilishwa katika Kiswahili Sanifu. Konsonanti zinazohawilishwa zimeoneshwu kwa kuzungushiwa duara. Konsonanti hizo ni /s/, /f/, na /l/ ambazo zinabainika katika maneno mbalimbali yaliyopo katika matini hiyo. Mifano Na. 6 na 7 inaonesha konsonanti /s/ ya Kihehe inayohawilishwa katika Kiswahili Sanifu.

Jedwali Na.2: Konsonanti /s/ Inayohawilishwa katika Kiswahili Sanifu

	Tahajia ya Neno	Matamshi katika Kihehe	Matamshi katika Kiswhili
6 (a)	zetu	/se:tu/	/ze:tu/
(b)	Ongezeko	/ɔŋgɛsɛ:kɔ/	/ɔŋgɛ'ze:ko/
7 (a)	hayakidhi	/ajaki:si/	/haja'kiði/
(b)	taadhima	/ta:si:ma/	/ta:ðima/

Chanzo: Data za Uwandani (2020)

Data Na. 6 na 7 zinaonesha matamshi ya fonimu /s/ ya Kihehe baada ya kuhawilishwa kwenda katika lugha ya Kiswahili Sanifu. Katika lugha ya Kiswahili, fonimu /s/ ya Kihehe hutamkwa kama fonimu /z/ kama ambayo inaonekana katika data Na. 6 (a) na (b). Uhawilishwaji mwingine wa fonimu /s/ ya Kihehe unabainika pia katika data Na 7 (a) na (b). Katika data hizo, ni dhahiri kuwa wajifunzaji huhawilisha /s/ ya Kihehe na kuiondoa fonimu /ð/ ya Kiswahili Sanifu kama ambavyo inaonekana katika mifano ya maneno Na. 7. Kama ilivyoelezwa awali kuwa, pamoja na kwamba fonimu /s/ ni mionganini mwa fonimu za Kiswahili Sanifu, wajifunzaji huitumia kwa namna tofauti na matumizi yake yaliyozoleka katika lugha ya Kiswahili Sanifu.

Tofauti na /s/, fonimu nyingine inayohawilishwa katika Kiswahili Sanifu ni /f/ ambayo inabainika katika maneno yaliyorodheshwa katika data Na. 8 (a) - (d). Katika data hiyo, imeoneshwa matamshi ya fonimu /f/ katika maneno ya lugha ya Kihehe na usahihi wake kimatamshi katika Kiswahili Sanifu:

Jedwali Na. 3: Konsonanti /f/ inayohawilishwa katika Kiswahili Sanifu

	Tahajia ya Neno	Matamshi katika Kihehe	Matamshi katika Kiswahili
8 (a)	vyumba	/fiju:mba/	/'vjumba/
(b)	viatu	/fijaa:tu/	/'vi:ja:tu/
(c)	vya	/fiya:/	/'vja:/
(d)	viti	/fi:ti/	/'viti/

Chanzo: Data za Uwandani (2020)

Data Na. 8(a) - (d) zinaonesha fonimu /f/ ya lugha ya Kihehe ambayo katika Kiswahili Sanifu hutamkwa kama fonimu /v/ kama ambavyo inaonekana katika data hiyo. Kufuatia mchakato wa uhawilishaji, fonimu /v/ ya Kihehe inapotokea katika neno la Kiswahili Sanifu, wajifunzaji huiondoa na kuiweka fonimu /f/ ya Kihehe.

Vilevile, fonimu nyingine iliyobainika kuhawilishwa ni /l/ katika maneno yafuatayo katika data Na. 9 (a) - (d):

Jedwali Na. 4: Konsonanti /l/ Inayohawilishwa katika Kiswahili Sanifu

	Tahajia ya Neno	Matamshi katika Kihehe	Matamshi katika Kiswahili
9 (a)	rasmi	/la:simi/	/'rasmi/
(b)	shukrani	/sukula:ni/	/'su'krani/
(c)	madarasa	/madala:sa/	/mada'ra:sa/
(d)	sekondari	/sekonda:li/	/seko'nda:ri/

Chanzo: Data za Uwandani (2020)

Katika data Na. 9 (a) - (d), tunabaini kuwa wajifunzaji hubadili matamshi sahihi ya Kiswahili Sanifu na kutamka kwa matamshi ambayo yamezoeleka katika lugha yao ya kwanza, yaani Kihehe. Tofauti ya baadhi ya fonimu baina ya Kihehe na Kiswahili Sanifu imekuwa ni moja ya sababu za uhawilishwaji wa fonimu za Kihehe katika Kiswahili Sanifu. Sababu nyingine zilizobainika ni umri wa wajifunzaji kuanza kujifunza L2; tofauti za mfumo wa fonolojia; ufundishaji wa lugha ya Kiswahili kama L2 kwa njia yenyeye kasoro; na baadhi ya walimu wanaofundisha somo la Kiswahili kukosa msingi mzuri wa lugha ya Kiswahili. Kwa mujibu wa data za utafiti huu, lugha ya Kihehe haina fonimu /ð/, /θ/, /ʒ/, /r/, /ʃ/ na /γ/ ambazo zinapatikana katika lugha ya Kiswahili Sanifu. Kukosekana kwa fonimu hizo ni moja ya sababu ya wajifunzaji wa lugha ya Kiswahili Sanifu kutumia fonimu nyingine mbadala (mathalani, fonimu /s/ hutumiwa badala

ya fonimu /ð/ /ʃ/ na /θ/: fonimu /l/ hutumiwa badala ya fonimu /r/) ili kufidia fonimu ya Kiswahili Sanifu isiyopatikana katika Kihehe.

Athari za uhawilishwaji wa fonimu za Kihehe katika ujifunzaji wa Kiswahili Sanifu

Matokeo ya utafiti yamebaini kwamba zipo athari mbalimbali zinazotokana na uhawilishaji wa fonimu za lugha ya Kihehe katika lugha ya Kiswahili. Athari hizo zimegawanyika katika makundi mawili. Kundi la kwanza linahusu athari zinazotokana na uhawilishwaji wa fonimu za irabu, na kundi la pili linahusu athari zinazotokana na uhawilishwaji wa fonimu za konsonanti.

Athari zinazotokana na uhawilishwaji wa fonimu za irabu

Irabu za Kihehe zenyе toni zinapohawilishwa katika Kiswahili Sanifu, huhawilishwa pamoja na toni zake. Uhawilishwaji huo husababisha athari katika maneno mbalimbali ya lugha hiyo. Data za utafiti wa makala hii zinaonesha athari zinazosababishwa na uhawilishwaji wa toni katika lugha ya Kiswahili Sanifu. Athari hizo ni urefushwaji wa matamshi ya irabu, na kuathiriwa kwa maana za maneno ya lugha ya Kiswahili Sanifu.

Urefushwaji wa matamshi ya irabu

Urefushwaji wa irabu ni mchakato wa kuifanya irabu ambayo awali ilikuwa fupi kuwa ndefu (Massamba, 2005). Akizungumzia dhana ya viarudhi katika lugha za Kibantu, Massamba (2005) anasema kuwa irabu fupi katika lugha nyingi za Kibantu zenyе toni hutamkwa kwa kurefushwa matamshi yake, jambo ambalo huathiri matamshi ya awali ya irabu hizo. Kwa mujibu wa Massamba (2004), urefushwaji wa irabu hauibadilishi irabu ambayo awali ilikuwa fupi na kuifanya kuwa ndefu, bali irabu ambayo ni fupi kwa asili yake hubakia kuwa fupi, kinachorefushwa ni matamshi yake tu. Kwa

mujibu wa data za utafiti wa makala hii, katika lugha ya Kihehe, toni husababisha urefushwaji wa matamshi ya irabu ambazo, kiasili, ni fupi. Data za utafiti huu zinaonesha kuwa irabu za Kihehe zinapohawilishwa katika lugha ya Kiswahili Sanifu, huhawilishwa pamoja na toni zake ambazo husababisha kurefushwa kwa matamshi yake. Data zifuatazo katika hadithi Na. 3 zinathibitisha hali hiyo.

Hadithi Na. 3

Apo samáni sá kále kulikuwépo na kijíji cha gangiluuísi. Katika kijíji icho kulikuwépo na wukówowa wátu wanaítwa mwakiomwíke. Mwakiomwíke alikuwa na tabía ya ofyo ya kupénda kutongósa tongósa wanawáke ofyo manjiyáni. Siku mója alikwénda kijiji cha mbáli kidógo njiyáni akakutána na bíndi muzúri muno. Akamupénda sána. Akamtongósa na akamuchukúwa adi kwáwo. Kufika kwáwo, akambíwa alipe ela nyíngi, mupíni mumója wa jémbe, debe la wùnga, sùka, akatembéya mwéndo muléfu kutafuta fitu alifyoagíswa. Alipolúdi, wale wakwe sáke wakaitána, walikaa kikáwo wakaséma kwakuwa amelípa sásá wacha amuchukúwe muke wáke. Akamuwówa yule mwanamúke. Wusíku bíndi yule akawondoka kimaajábu tu kulúdi kwáwo ...

Chanzo: Data za Uwandani (2020)

Hadithi Na. 3 inaonesha maneno mbalimbali ya Kiswahili Sanifu yaliyorefushwa kimatamshi kufuatia irabu zenye toni zilizohawilishwa katika lugha hiyo. Data Na. 10 na 11 zinaonesha baadhi ya maneno hayo yakiwa katika maandishi yake ya kawaida, na katika matamshi ya lugha ya Kihehe na usahihi wake kimatamshi katika lugha ya Kiswahili Sanifu:

Jedwali Na. 5: Irabu za Kiswahili Sanifu Zilizorefushwa Matamshi

Tahajia ya Neno	Matamshi ya Kihehe	Matamshi ya Kiswahili Sanifu
10(a) zamani	/sama:ni/	/za'mani/
(b) lilanza	/lilia:za/	/lili'anza/
(c) kazi	/ka:si/	/'kazi/
11(a) zote	/so:te/	/'zote/
(b) kutongoza	/kutongo:sa/	/kuto'ngoza/
(c) za	/sa:/	/za/

Chanzo: Data za Uwandani (2020)

Data Na. 10 na 11 zinaonesha maneno mbalimbali ya Kiswahili Sanifu yakiwa katika matamshi ya Kihehe (yenye toni) katika baadhi ya silabi. Data hizo zinaonesha maneno hayohayo yakiwa katika matamshi ya Kiswahili Sanifu. Utafiti huu umebaini kuwa silabi zilizobeba toni katika maneno yaliyorefushwa matamshi, hutamkwa kwa kusikika zaidi ukilinganisha na silabi nyingine katika neno. Kwa mujibu wa data za utafiti huu, uhawilishaji wa toni katika Kiswahili Sanifu husababisha athari za kimatamshi katika maneno ya lugha ya Kiswahili Sanifu ambayo kiasili si lugha yenye toni. Katika Kiswahili Sanifu, maneno hayatamkwi kwa kurefusha fonimu za irabu kama yanavyotamkwa katika lugha ya Kihehe. Hivyo, uhawilishwaji wa fonimu zenye toni husababisha maneno ya lugha hiyo pia yatamkwe kwa kurefushwa zaidi matamshi kama iliyo katika lugha ya Kihehe. Data za utafiti huu zinaonesha kuwa kuna uhusiano wa karibu baina ya toni na urefushwaji wa matamshi ya irabu katika lugha ya Kihehe. Kwa mujibu wa matokeo ya utafiti huu, irabu zenye toni zimeonekana kutamkwa kwa kurefushwa zaidi matamshi yake ukilinganisha na irabu nyingine zisizokuwa na toni.

Kuathiriwa kwa maana za maneno

Athari nyingine ya uhawilishwaji wa irabu za Kihehe zenyé toni katika Kiswahili Sanifu ni kuathiriwa kwa maana ya maneno. Mbali na athari za kimatumshi, uhawilishaji wa toni katika Kiswahili Sanifu husababisha athari za kimaana. Mabadiliko ya neno kimaana huathiri ujumbe ambao umekusudiwa kumfikia mpokeaji aliyelengwa na msemaji. Kama ilivyoelezwa awali kuwa lugha ya Kiswahili kwa asili yake ni lugha isiyokuwa na toni, uhawilishaji wa toni katika lugha hiyo husababisha maneno yatamkwe kwa kurefusha matamshi, jambo ambalo huathiri matamshi ya neno husika. Hili linathibitishwa na data zifuatazo zilizopatikana kwa njia ya masimulizi ya hadithi.

Hadithi Na. 4

Sukuláni ya Púnda ni Mateeke

“...Símba alimfwatilíya sána súngula kwa sabábu waliwésa kuula na kusíba fiyákula fiyáwo. Hifohifo sámu ya símba ilifíka ya kuwínda polní kutafúta fyákula... Siku yíngi símba alisíndwa kuwénda polní kutafuta fiyákula kwa sabábu alikuwa anawúmwa kiyási kwámba akuwésa kuwa na ngúfu sákuwínda polní...”

Chanzo: Data za Uwandani (2020)

Hadithi Na. 4 inaonesha maneno mbalimbali ya Kiswahili Sanifu ambayo yana toni iliyohawilishwa pamoja na maneno hayo kutoka katika lugha ya Kihehe. Tunaweza kuyaona maneno hayo na jinsi yanavyotamkwa na wajifunzaji lugha katika data Na. 12 na 13.

Jedwali Na. 5: Maneno ya Kiswahili Sanifu Yaliyorefushwa Matamshi

Tahajia ya Neno	Matamshi ya Kihehe	Matamshi ya Kiswahili Sanifu
12 (a) zamu	/sa:mu/	/'zamu/
(b) nguvu	/ŋgu:fu/	/'ŋguvu/
(c) kiasi	/kija:si/	/ki'asi/
13 (a) hakuweza	/akuwe:sa/	/haku'weza/
(b) vyao	/fiya:wɔ/	/'vyao/
(c) za	/sa:/	/za/

Chanzo: Data za Uwandani (2020)

Data Na. 12 na 13 inaonesha maneno mbalimbali ya Kiswahili Sanifu na matamshi yake katika Kihehe na lugha ya Kiswahili Sanifu. Tukirejea katika data hiyo, tunaona kuwapo kwa mabadiliko ya maneno kiumbo na kimatamshi. Mabadiliko ya maneno hayo kimatamshi yameathiri maana sahihi ya maneno hayo ya lugha ya Kiswahili, mathalani neno la Kiswahili Sanifu <kiasi> lenye maana ya hali ya kiwango kisicho cha juu wala cha chini (wastani) wajifunzaji hulitamka kama <kiyaasi> neno ambalo si la Kiswahili Sanifu na halina maana katika lugha hiyo. Vilevile, neno <vy> linalotumika kuhusisha nomino ya ngeli ya ki/vi na nomino au neno jingine wajifunzaji hulitamka kama <fy> neno ambalo halina maana katika lugha ya Kiswahili Sanifu.

Mbali na maneno hayo, neno <za> linalotumika kuhusisha nomino ya ngeli ya i/zi na nomino nyingine wajifunzaji hulitamka kama <saa> lenye maana ya chombo maalumu cha kuonesha muda ambayo ni maana tofauti na ya neno la awali. Neno jingine ni <zamu> lenye maana ya namna ya kufanya kazi au jambo fulani kwa kupokezana kila mmoja akiwa na kipindi chake ambalo wajifunzaji hulitamka kama <saamu> neno ambalo si la Kiswahili Sanifu na halina maana katika lugha hiyo. Mbali na maneno hayo, neno jingine ni <vyawo> lenye maana ya kimiliki cha nafsi ya tatu wingi kikionesha nomino inayomilikiwa iko katika ngeli ya ki/vi. Kuathiriwa kwa maana za maneno kama hayo huathiri ujumbe ambao umekusudiwa kumfikia mpokeaji aliyelengwa na msemaji. Jambo hilo hutatiza mawasiliano baina ya wazungumzaji wa lugha hiyo.

Athari zinazotokana na uhawilishwaji wa fonimu za konsonanti za Kihehe

Mbali na kuathiriwa kwa maana za maneno kutokana na uhawilishaji wa fonimu tofauti, matokeo ya utafiti yameonesha kuwa uhawilishwaji wa konsonanti za Kihehe husababisha mabadiliko katika baadhi ya fonimu za Kiswahili Sanifu. Imedhihirika kuwa mabadiliko hayo ya fonimu husababishwa na mchakato wa ubadilishanaji wa fonimu unaofanywa na wajifunzaji lugha wanapokuwa katika mchakato wa kujifunza lugha. Katika kipengele hiki, tutawasilisha data kuhusu ubadilishanaji wa konsonanti za Kihehe na Kiswahili Sanifu, kisha tutaona namna mchakato huo unavyosababisha mabadiliko ya fonimu za konsonanti za Kiswahili Sanifu.

Ubadilishanaji wa fonimu za konsonanti za Kihehe na Kiswahili Sanifu

Ubadilishanaji wa fonimu ni mbinu ya kuiweka fonimu fulani katika nafasi ambayo fonimu nyingine iliyosababisha amba na fonimu ya awali katika neno kutokuwapo katika mfumo wa fonolojia wa lugha fulani au makosa yanayosababisha na athari za L1. Data za utafiti huu zinaonesha kuwa ubadilishanaji wa fonimu baina ya Kihehe na Kiswahili Sanifu husababishwa na mambo yote mawili, yaani baadhi ya fonimu za Kihehe kutokuwapo katika lugha ya Kiswahili Sanifu na makosa yanayosababisha na athari za L1. Katika utafiti huu, ubadilishanaji wa fonimu umedhihirika zaidi kupitia mbinu ya usimulizi wa hadithi na jaribio lililokuwa na maswali ya orodha chunguzi. Zifuatazo ni data zilizokusanywa kwa njia ya usimulizi wa hadithi kuonesha namna mchakato wa ubadilishaji wa fonimu unavyofanywa na wajifunzaji lugha.

Hadithi Na. 5

Hadithi ya Kuku na Kwale

“Adiisi adiisi. Apo samaani saa kaale, kuku na kwaale walikuwa malafiiki ambaawo walikuwa wanaiisi pamooja. Siku mooja walieenda kuwiinda paazi walipaata paazi wataano. Kuku alimwambiya kwaale leete awo paazi miimi nikachoome kwenye iile nyumba ya musee joobu. Kwale akakubaali kiisa kuku akachukuua wale paazi akaeenda kuchoma na akala woote. Baada ya kumaliisa kula hakuluudi tena poliini. Kwaale akaaza kumuwiita kuku, akasema “kuku we” kuku wee, kuku wee! Kuku akajiibu kamewunguuwa! Taangu siku iyo ulafiiki wa kuku na kwaale ukaisiia apo na atimaaye kuku anaiisi nyumbaani na binadaamu na kwale anaiisi poliini.”

Chanzo: Data za Uwandani (2020)

Hadithi Na. 5 inaonesha maneno mbalimbali yaliyopitia mchakato wa ubadilishaji wa fonimu unaofanywa na wajifunzaji wa Kiswahili Sanifu wa jamii ya Wahehe. Kupitia data hiyo, tunabaini ubadilishanaji wa fonimu katika maneno yafuatayo:

Jedwali Na. 7: Ubadilishanaji wa Fonimu za Kihehe na Kiswahili Sanifu

Tahajia ya Neno	Matamshi katika Kihehe	Matamshi katika Kiswahili
14(a) zamani	/sama:ni/	/za'mani/
(b) mzee	/muse:ε/	/m'zee/
(c) za	/sa:/	/za/
15(a) marafiki	/malafi:ki/	/mara'fiki/
(b) hakurudi	/akulu:di/	/haku'rudi/
(c) porini	/poli:ni/	/po'rini/
16(a) hadithi	/adi:si/	/ha'diθi/
(b) kasha	/ki:sə/	/kifa/
(c) anaishi	/anai:si/	/ana'iʃi/

Chanzo: Data za Uwandani (2020)

Data Na. 14 - 16 zinaonesha ubadilishanaji wa fonimu katika maneno mbalimbali ya Kihehe na Kiswahili Sanifu. Katika data hizo, tunaona ubadilishanaji wa fonimu /z/ ya Kiswahili Sanifu na /s/ ya Kihehe, hususani katika data Na. 14 (a) - (c). Vilevile, fonimu /r/ inabadilishana nafasi na fonimu /l/ katika data Na. 15 (a) - (c). Fonimu /θ/ inabadilishana nafasi na fonimu /s/ katika data Na. 16 (a). Tofauti na ubadilishanaji huo, fonimu /ʃ/, inabadilishana nafasi na fonimu /s/ katika data Na. 16 (b) na (c).

Mabadiliko ya konsonanti za Kiswahili Sanifu katika mchakato wa ujifunzaji lugha

Utafiti huu umedhihirisha kwamba mchakato wa ubadilishanaji wa fonimu husababisha mabadiliko katika baadhi ya fonimu za Kiswahili Sanifu. Kufuatia mchakato huo, fonimu zilizobadilika ni /z/ /v/ /r/ /ʃ/ /ð/ /θ/. Mabadiliko hayo ya konsonanti ni mojawapo ya athari zinazoikumba lugha ya Kiswahili Sanifu na kuathiri wajifunzaji lugha katika mchakato wa ujifunzaji. Tunaweza kuona mabadiliko hayo kuitia data ambazo zimepatikana kwa njia ya jaribio walilofanya, kama zinavyowasilishwa katika Kielelezo Na. 2.

Kielelezo Na. 2: Jaribio

Namba	Kihehe	Kiswahili Sanifu
1	Umulyaango gwaangu gwadeenyike chaaka	Mulaainge waangu uli finjiika ibaaya
2	Mugogolo akuusa ukoota umooto	Mujee arakunja kumoto
3	Mnya kaaye aasa ipa milaau na fingeamba	Minyenyenye mtaa atekunja keeso na filyaa
4	Mweenda gwaangu munofu hiilo	Mgwayaangu sunsi sene
5	Iimbwa yaalye mnyamuguunda	Uimbwa ilikula ture ngesa amba
6	Iliino lyaangu liivava	Iliino laangu Unawumia
7	akwanaanga Mutuka	Anaqibu gaell
8	Vahiisile lisaaati la suule	Wahieebi saab la
9	Nnzoka imulumite mu Liiho	Nzoruka inayuhuru na masoomi
10	Sawaadi aleemaa ukweegala mwaana yuungi	Sawaadi pateeki ku baabutobetee na
11	Afweete isookisi na filaaatu fya suule	Amefanya saakisti na fyaat fya a suule
12	Ikaaye yaneene yaagwe idaaha hiilo	Miyumba ya miliini
13	Mbeva silye mangoogo mbegaali	Panya silikuula kala anga Route
14	Wuse taandi	Uuje kwaara
15	Ifikoombe fiduung'u si fya neene	Ifikoombe Ayekun-hatu si ha
16	Isiiki sinyauhulo	Sidq Si a jaabu
17	Ifiilatu fyaangu fitiitu fyayaasile daaha hiilo	Fiatu fyaangu five fitiito daa samaani
18	Ikisaasi cha neeng'uni kigaya mmigo	Kisasi cha leo akina ka
19	Unyoko vaangu afwile kuinji savaanu	Ina ma wa miliini anefati kilei inji sa waabu
20	Udeeniyite ikitaanda cha samaani	Umeshunja kitaenda cha samaani
21	Amtofile mwaana	Cameru piga mudiado
22	Umuyaango afweete mweenda munofu	Mweesaangano fwa ngudo Swidi
23	Masaaka iilowa soomba	Masaaka ana fwa Sa raaki
24	Agusile lisulia na Isaala	Alizunewa Se isaala
25	Woopole myeenda ja vaana	Woopole wosha me

Chanzo: Data za uwandani (2020)

Kielelezo Na. (2) kinaonesha ubadilikaji wa fonimu za konsonanti za Kiswahili baada ya mchakato wa uhawilishwaji kufanyika. Katika maneno hayo, konsonanti za Kihehe zimezungushiwa duara. Tukirejea katika data hizo, tunaona kuwa wajifunzaji lugha huitamka fonimu /z/ ya Kiswahili Sanifu kama /s/. Ubadilishaji huo wa fonimu huiathiri lugha ya Kiswahili kimamatamshi na kimaana pia. Tunaweza kuona mabadiliko hayo ya fonimu katika data Na. (17).

Jedwali Na. 8: Mabadiliko ya Konsonanti /z/ ya Kiswahili Sanifu

	Tahajia ya Neno	Matamshi katika Kihehe	Matamshi katika Kiswahili
17 (a)	mzee	/muse:/	/mze:/
(b)	viazi	/fija:si/	/vi'a:zi/
(c)	zote	/so:te/	/zote/
(d)	kizazi	/kisa:si/	/ki'za:zi/

Chanzo: Data za Uwandani (2020)

Data Na. 17 (a) - (d) zinaonesha konsonanti /s/ ya Kihehe inayohawilishwa katika Kiswahili Sanifu. Katika mifano hiyo, fonimu /s/ imewekwa katika matamshi yake sahihi ya Kihehe, maandishi yake ya kawaida na matamshi yake sahihi katika Kiswahili Sanifu. Mabadiliko ya konsonanti /z/ yanmetokea upande wa lugha ya Kiswahili kwa sababu matamshi sahihi ya fonimu hiyo katika Kiswahili Sanifu ni /z/ na si /s/ kama inavyobainika katika data hiyo. Mbali na hayo, mabadiliko mengine ni ya fonimu /v/ ya Kiswahili Sanifu ambayo wajifunzaji huitamka kama /f/. Tukirejea katika Jedwali Na. 10, tunaona mabadiliko ya fonimu /f/ katika maneno yaliyoorodheshwa katika data Na. 18 (a) - (d).

Jedwali Na. 10: Mabadiliko ya Konsonanti /v/ ya Kiswahili Sanifu

	Tahajia ya Neno	Matamshi katika Kihehe	Matamshi katika Kiswahili
18(a)	ulivunjika	/ulifupji:ka/	/ulivu'njika/
(b)	vibaya	/fiba:ja/	/vi'baja/
(c)	viatu	/fijaa:tu/	/vi'ja:tu/
(d)	amevaa	/amefwa:/	/a'meva:/

Chanzo: Data za Uwandani (2020)

Data Na. 18 (a) - (d) zinaonesha fonimu /f/ ya Kihehe katika maneno mbalimbali na jinsi inavyopaswa kutamkwa katika lugha ya Kiswahili Sanifu.

Tofauti na fonimu hizo, mabadiliko mengine ni ya fonimu /r/ ya Kiswahili Sanifu ambayo wajifunzaji huibadili na huitamka kama /l/. Mifano Na. 19 (a) - (d) inaonesha mabadiliko hayo kama ambavyo inaonekana katika Jedwali Na. 11.

Jedwali Na. 11: Mabadiliko ya konsonanti /r/ ya Kiswahili Sanifu

	Tahajia ya Neno	Matamshi katika Kihehe	Matamshi katika Kiswahili
19 (a)	nzuri	/su:li/	/'nzuri/
(b)	gari	/liga:li/	/'ga:ri/
(c)	amefariki	/amefaliki:a/	/amefa'riki/
(d)	anaharibu	/anaali:bu/	/anaha'ribu/

Chanzo: Data za Uwandani (2020)

Data Na. 19 (a) - (d) zinaonesha fonimu /l/ ya Kihehe katika maandishi ya kawaida na matamshi yake katika lugha ya Kihehe na Kiswahili Sanifu.

Mabadiliko mengine ni ya fonimu /ð/ ambayo hubadilika na kuwa /s/. Mabadiliko haya yanathibitishwa na kielelezo Na. (3) cha jaribio kifuatacho.

Kielelezo Na. 3: Jaribio

28	<i>Ihela</i>	aana
29	<i>Wopole</i>	fuua
30	<i>Idaaha</i>	saraani
31	<i>Nndatu</i>	fyaaku
32	<i>ifito</i>	fitto
33	<i>Weegale</i>	saa
34	<i>Kemeele</i>	lta
35	<i>Mwaana</i>	mutoto
36	<i>Isala</i>	saala
37	<i>Ikilsa</i>	lisa
38	<i>Isaamhi</i>	saambi
39	<i>Ifinu</i>	fitu
40	<i>Kweege</i>	fuuka
41	<i>Umutuka</i>	gaali
42	<i>Aale</i>	ayaya
43	<i>mahoosa</i>	mawooso
44	<i>Kaangasee</i>	kaasa
45	<i>Hulula</i>	fuusa
46	<i>Sulu</i>	suulu
47	<i>Ikaasi</i>	kaasi
48	<i>Malaasi</i>	malaa(s)i
49	<i>Ikula</i>	ku
50	<i>Inchi</i>	inji

28	Ihela	aana
29	Wopole	fuuua
30	Idaaha	saaanl
31	Nndatu	fiyaaku
32	ifito	filto
33	Weegafe	saa
34	Kemeele	itta
35	Mwaama	Mutoto
36	Isala	-saala
37	Ikilsa	Viisa
38	Isaambi	Saambi
39	Ifinu	filku
40	Kweego	Fuuta
41	Umutuka	gaali
42	Aale	oraya
43	mahoosa	mawooso
44	Kaangasee	kansa
45	Hulula	fuujo
46	Sulu	Shuru
47	Ikaasi	Kaasi
48	Malaasi	malan(s)
49	Ikula	ku
50	Inchi	inji

Chanzo: Data za Uwandani

Data katika kielelezo Na. (3) cha jaribio zinaonesha mabadiliko ya fonimu /ð/ ambayo hubadili na kuwa fonimu /s/. Data zifuatazo zinaonesha fonimu /ð/ ikiwa katika maandishi yake ya kawaida kabla ya uhawilishwaji na matamshi yake katika lugha ya Kihehe. Data hiyo inaonesha matamshi

ya fonimu hiyo katika lugha ya Kiswahili Sanifu kuitia maneno ambayo yamechukuliwa kutoka katika Jedwali Na. 12.

Jedwali Na.12: Mabadiliko ya Konsonanti /ð/ ya Kiswahili Sanifu

	Tahajia ya Neno	Matamshi katika Kihehe	Matamshi katika Kiswahili
20 (a)	dhambi	/sa:mbi/	/'ðambi/
(b)	dhuru	/su:lu/	/'ðuru/
(c)	maradhi	/mala:si/	/ma'raði/

Chanzo: Data za Uwandani (2020)

Data Na. 20 (a) - (c) zinaonesha fonimu /ð/ katika maandishi yake ya kawaida katika lugha ya Kiswahili na matamshi yake katika lugha ya Kihehe na Kiswahili Sanifu kabla ya uhawilishwaji.

Mabadiliko mengine ni ya fonimu /θ/ ya Kiswahili Sanifu ambayo wajifunzaji hutamka kama fonimu /s/. Tunaweza kuona mabadiliko hayo katika data Na. (21) zilizomo katika Jedwali Na. 13.

Jedwali Na.13: Mabadiliko ya Konsonanti /θ/ ya Kiswahili Sanifu

	Tahajia ya Neno	Matamshi katika Kihehe	Matamshi katika Kiswahili
21 (a)	theluji	/selu:ji/	/θe'laji/
(b)	thamani	/sama:ni/	/θa'ma:ni/

Chanzo: Data za Uwandani (2020)

Katika data Na. 21 (a) - (b), tunaona fonimu /θ/ ya Kiswahili Sanifu inavyobadilishwa na wajifunzaji wa lugha na kuitamka kama /s/. Wajifunzaji hao hufanya mabadiliko haya ya fonimu kwa sababu hawana usuli na fonimu /θ/ ambayo si mionganini mwa fonimu za lugha ya Kihehe. Fonimu nyingine inayokumbwa na mabadiliko ni /ʃ/ ya Kiswahili Sanifu ambayo wajifunzaji huitamka kama /s/. Tunaweza kuiona fonimu /ʃ/ ikiwa

katika matamshi ya lugha ya Kihehe na jinsi inavyopaswa kutamkwa katika lugha ya Kiswahili Sanifu katika data Na. 22 (a) - (c) za Jedwali Na. 14.

Jedwali Na.14: Mabadiliko ya Konsonanti /ʃ/ ya Kiswahili Sanifu

	Tahajia ya Neno	Matamshi katika Kihehe	Matamshi katika Kiswahili
22(a)	Kesho	/kɛ:sɔ:/	/'kɛʃɔ:/
(b)	Shule	/su:le /	/'su:le/
(c)	Shuka	/su:ka/	/'su:ka/

Chanzo: Data za Uwandani (2020)

Data Na. 22 (a) - (c) zinaonesha matamshi ya fonimu katika lugha ya Kihehe na usahihi wake wa matamshi katika lugha ya Kiswahili Sanifu. Kama ilivyo kwa /ð/ na /θ/, fonimu /ʃ/ pia hubadilishwa na /s/ ya Kihehe kwa sababu si mionganini mwa fonimu katika lugha ya Kihehe.

Wajifunzaji lugha hubadili fonimu za Kiswahili Sanifu na kutamka kwa matamshi ambayo yamezoleka katika lugha yao ya kwanza. Ubadirishaji huo wa fonimu huyaathiri maneno ya Kiswahili Sanifu kimatamshi na kimaana. Kwa mfano, tukirejea katika data Na. 14 tunabaini mabadiliko ya neno <thamani> na kuwa <samani>. Neno <thamani>, kwa mujibu wa BAKITA (2017), lina maana ya ubora wa kitu unaotokana na umuhimu na kuhitajika kwake na jamii, na neno <samani> humaanisha vyombo vilivyoumbwa kwa mbao, plastiki, miti, miyaa na kadhalika. Pia, neno <zamani> lenye maana ya kitambo cha miaka mingi iliyopita wajifunzaji hulibadilisha na kuwa <samani> lenye maana sawa na iliyotolewa hapo juu. Vilevile, katika Mfano Na. 17 (a), neno <kizazi> lenye maana ya watu au viumbe walioishi kipindi fulani cha historia hubadilishwa na kutamkwa kama <kisasi> likiwa na maana ya dhamira, nia au kusudio la kulipiza ubaya uliotendwa. Tukirejea katika maneno hayo, tunaona kuwa maana za

maneno hayo ni tofauti na maana za maneno ya awali. Ni dhahiri kuwa mabadiliko haya ya maana yanaathiri ujumbe kwa kuwa maana itakayomfikia msikilizaji si ile iliyokusudiwa na mtoaji wa ujumbe.

Hitimisho

Utafiti huu ulihusu uhawilishaji wa fonimu za Kihehe na athari zake katika ujifunzaji wa Kiswahili sanifu. Matokeo ya utafiti huu yamebainisha athari za namna tatu. Kwanza, ni urefushwaji wa matamshi. Pili ni kuathiriwa kwa maana za maneno na tatu ni mabadiliko ya Baadhi ya fonimu za Kiswahili Sanifu. Uwasilishaji, uchanganuzi na ufasiri wa data za utafiti huu wa makala umefanywa kwa kuzingatia msingi wa NUL unaohusu ubainishaji wa vipengele vya L1 vinavyohamishiwa katika L2 katika mchakato wa ujifunzaji lugha na athari zake. Kwa kutumia msingi huu, vipengele vya fonolojia ya Kihehe vinavyohawilishwa katika ujifunzaji wa Kiswahili Sanifu kama L2 vimeweza kubainishwa. Vilevile, kuititia msingi huu, athari za uhawilishwaji wa fonimu za Kihehe katika Kiswahili Sanifu zimebainishwa. Kufuatia athari zilizobainishwa, makala hii inapendekeza mbinu zitakazosaidia kupunguza athari za uhawilishwaji wa fonimu za Kihehe katika ujifunzaji wa Kiswahili Sanifu kama lugha ya pili (L2). Mbinu mojawapo ni wajifunzaji lugha kufanya mazoezi ya kutosha ya somo la Kiswahili ambayo yatasaidia kuboresha matamshi yao.

Marejleo

BAKITA. (2017). *Kamusi Kuu ya Kiswahili*. Dar es Salaam: Longhorn Publishers Limited.

Kanake, K.J. (2013). Makosa ya Kifonolojia Miongoni mwa Wanafunzi wa Kiigembe katika Ujifunzaji Lugha ya Kiswahili, (Tasinifu ya Uzamivu, haijachapishwa), Chuo Kikuu cha Kenyatta.

Khamis, M. (2012). Athari za Matamshi ya Msamiati wa Kiswahili Sanifu katika Kimakunduchu (Tasinifu ya Umahiri, haijachapishwa), Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

Kileo, G, J. (2017). Athari za Kimofofonolojia za Kiswahili katika Lugha ya Kihaya. (Tasinifu ya Umahiri, haijachapishwa), Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

Lado, R. (1957). *Linguistics Across Cultures*. Michigan: The University of Michigan Press.

Madumulla, J.S. (1995). *Proverbs and Sayings: Theory and Practice*. Dar es Salaam: TUKE.

Massamba, D.P.B. (1986). On the Influence of Local Languages on Kiswahili: The Case of Mara Region in Tanzania. *Kiswahili*, 53(1) na 53(2), 67 - 83.

Massamba, D.P.B. (2004). *Kamusi ya Isimu na Falsafa ya Lugha*. Dar es Salaam: TUKE.

Massamba (2005). The Role of Suprasegmental Phenomena in the Analysis of Bantu Languages: With Special Reference to Ciruuli. *In Occasional Papers in linguistics*: University of Dar es Salaam.Tanzania.

Mochiwa, Z.M. (1979). The Impact of Kiswahili Language on Ethnic Languages: A Case Study from Handeni District, (Tasinifu ya Umahiri, haijachapishwa), Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

Myles, na Mitellell, R (2004). *Second Language Learning Theories*. Second Edition Hodder Arnold, an Imprint of Hodder Education.

Mukuthuria, M. (2004). Kuathiriana kwa Kiswahili na Kimeru: Mfano kutokana na Wanafunzi wa Kitigania, Kenya, (Tasinifu ya Uzamivu, hajachapishwa), Chuo Kikuu cha Egerton.

Obuchi, S.M. & Mukhwana, A. (2015). *Muundo wa Kiswahili Ngazi na Vipengele*. Jomo Kenyatta Foundation: Nairobi Kenya.

Rubanza, Y.I. (1979). The Relationship between Kiswahili and other African Languages: The Case of Kihaya, (Tasinifu ya Umahiri, hajachapishwa), Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

TUKI (1990). Kamusi Sanifu ya Isimu na Lughu. Dar es Salaam: TUKI.